TANGAZO LA SERIKALI NA. 807 la tarehe 13/9/ 2024

SHERIA YA MISITU,
(SURA YA 323)

KANUNI

(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 106(1)(aa))

KANUNI ZA UTARATIBU WA USAFIRISHAJI WA VENIA KWENDA NJE YA NCHI ZA MWAKA 2024

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Utaratibu wa Usafirishaji wa Venia Kwenda Nje ya Nchi za Mwaka 2024.

Tafsiri

2. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahita vinginevyo-

"Kamishna wa Uhifadhi" maana yake ni Kamishna wa Uhifadhi wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania;

Sura ya 323

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Misitu;

"venia" maana yake ni kipande chembamba kilichomenywa kutoka kwenye gogo ambacho hutumika kuzalisha bidhaa mbalimbali;

TS. Na. 269 la 2010

"Wakala" maana yake ni Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania ulioanzishwa chini ya Amri ya Uanzishwaji wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania; na

"Waziri" ina maana iliyotolewa katika Sheria.

SEHEMU YA PILI
UTARATIBU WA USAFIRISHAJI WA VENIA KWENDA NJE YA NCHI

Katazo la kusafirisha venia

3. Mtu hatasafirisha venia kwenda nje ya nchi bila kupata kibali kutoka kwa Kamishna wa Uhifadhi kitakachotolewa baada ya kupata ridhaa ya Waziri.

Utaratibu wa maombi ya kibali cha kusafirisha venia

4.-(1) Mtu anayekusudia kusafirisha venia kwenda nje ya nchi atatakiwa kuomba kibali kwa Kamishna wa Uhifadhi kwa kujaza Fomu Namba 1 iliyoainishwa katika Jedwali akiainisha kiasi cha mita za ujazo anazoomba.

(2) Maombi ya kibali cha kusafirisha venia kwenda

nje ya nchi yaliyoainishwa katika kanuni ndogo ya (1) yatatakiwa kuambatana na nyaraka zifuatazo:

(a) cheti cha usajili wa kampuni;
(b) cheti cha usajili wa namba ya Utambulisho ya Mlipa Kodi;
(c) cheti cha usajili wa biashara ya mazao ya misitu;
(d) leseni ya biashara kwa ajili ya kusafirisha mazao ya misitu kwenda nje ya nchi kutoka kwenye Mamlaka husika;
(e) cheti cha uthibitisho wa mlipakodi;
(f) hati ya usajili wa kiwanda cha kuzalisha venia;
(g) iwapo ni mwombaji wa mara ya kwanza, mpango wa uwekezaji unaoainisha namna ya kubadili teknolojia kwa ajili ya kuzalisha mazao ya misitu yaliyohandisiwa na utekelezaji wake; na
(h) iwapo ni mwombaji wa mara ya pili na kuendelea, taarifa ya utekelezaji wa mpango wa uwekezaji ulioainishwa katika aya ya (g).

Uchakataji wa maombi

5.-(1) Kamishna wa Uhifadhi atachakata maombi yaliyowasilishwa chini ya kanuni ya 4 kwa lengo la kujiridhisha endapo mwombaji amekidhi masharti yaliyoainishwa katika kanuni ya 4.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1) Kamishna wa Uhifadhi atajiridhisha endapo taarifa ya utekelezaji iliyowasilishwa kwa mujibu wa kanuni ya 4(2)(g) inaakisi maendeleo ya utekelezaji wa mpango wa uwekezaji.

(3) Kamishna wa Uhifadhi baada ya kuchakata maombi atawasilisha mapendekezo yake kwa Waziri kwa ajili ya kupata ridhaa.

(4) Baada ya Waziri kupokea mapendekezo ya kutolewa kibali chini ya kanuni ndogo ya (1), anaweza kwa maandishi-

(a) kuridhia kutolewa kwa kibali; au
(b) kutoridhia kutolewa kwa kibali na kueleza sababu za uamuzi huo.

(5) Baada ya Waziri kuridhia kutolewa kwa kibali cha usafirishaji wa venia kwenda nje ya nchi, Kamishna wa Uhifadhi, atatoa kibali cha kusafirisha venia kwenda nje ya nchi katika Fomu Namba 3 iliyoainishwa katika Jedwali.

(6) Endapo Waziri hataridhia kutolewa kwa kibali cha usafirishaji wa venia kwenda nje ya nchi, Kamishna wa Uhifadhi, atamjulisha mwombaji kutoridhiwa kwa maombi yake akiainisha sababu zilizobainishwa na Waziri.

Cheti cha usafirishaji wa

6.-(1) Mtu mwenye kibali cha kusafirisha venia

venia na ukaguzi wa shehena

atapaswa kuwasilisha maombi ya kupatiwa cheti cha usafirishaji na ukaguzi wa kila shehena ya venia inayokusudiwa kusafirishwa kwenda nje ya nchi kutoka kwa Kamishna wa Uhifadhi kwa kutumia Fomu Namba 2 iliyoainishwa katika Jedwali.

(2) Kamishna wa Uhifadhi, baada ya kupokea maombi yaliyowasilishwa katika kanuni ndogo ya (1), atafanya ukaguzi wa shehena ya venia inayokusudiwa kusafirishwa kwenda nje ya nchi ili kujiridhisha na taarifa zilizotolewa na mwombaji.

(3) Baada ya kujiridhisha na taarifa za shehena ya venia inayokusudiwa kusafirishwa kwenda nje ya nchi, Kamishna wa Uhifadhi atatoa Cheti cha Ukaguzi na Cheti cha Kusafirisha venia kwenda nje ya nchi kwa kutumia Fomu Namba 4 na 5 kama zilivyoainishwa katika Jedwali.

Ada ya usafirishaji wa venia kwenda nje ya nchi

7. Mtu anayesafirisha venia kwenda nje ya nchi atatakiwa kulipa kwa Wakala ada ya usafirishaji wa venia kwenda nje ya nchi ambayo ni asilimia tano ya thamani ya shehena ya venia inayosafirishwa kwenda nje ya nchi.

SEHEMU YA TATU
MASHARTI MENGINEYO

Taarifa ya utekelezaji

8. Kamishna wa Uhifadhi kila baada ya miezi mitatu, atawasilisha kwa Waziri taarifa ya kina ya utekelezaji wa Kanuni hizi ikiainisha-

(a) idadi ya vibali vilivyotolewa;

(b) utekelezaji wa mpango wa uwekezaji wa namna ya kubadili teknolojia kwa ajili ya kuzalisha mazao ya misitu yaliyohandisiwa kwa wote waliopatiwa vibali vya kusafirisha venia kwenda nje ya nchi;

(c) ujazo wa venia iliyotolewa kibali kusafirishwa kwenda nje ya nchi; na

(d) thamani ya venia iliyotolewa kibali kusafirishwa kwenda nje ya nchi.

Muda wa matumizi ya Kanuni hizi

9.-(1) Kanuni hizi zitatumika kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia tarehe ya kuchapishwa katika Gazeti la Serikali.

(2) Baada ya muda wa matumizi ya Kanuni hizi kufika ukomo, mtu yeyote hataruhusiwa kusafirisha venia kwenda nje ya nchi.

JEDWALI

(Limetengenezwa chini ya kanuni za 4(1), 5(5), 6(1) na 6(3))

FOMU NAMBA 1

FOMU YA MAOMBI YA KIBALI CHA USAFIRISHAJI WA VENIA KWENDA NJE YA NCHI

Mimi/Sisi ninaomba/tunaomba kibali cha kusafirisha Venia kwenda nje ya Nchi.

1. Jina la Kampuni: ……
2. Anuani: …… Namba ya simu: …….
3. Barua Pepe: ……..
4. Kiwango kwa Mita za Ujazo: .....

Jina la Mwombaji: …….

Wadhifa: ……..
Saini: ……
Tarehe: …….
Muhuri wa Kampuni: …….

FOMU NAMBA 2

FOMU YA MAOMBI YA CHETI CHA USAFIRISHAJI/UKAGUZI WA VENIA KWENDA NJE YA NCHI

Mimi/Sisi ninaomba/tunaomba cheti cha usafirishaji/ukaguzi wa venia kwenda nje ya Nchi.

1. Jina la Kampuni: ……
2. Anuani: ……Namba ya simu: ……..
3. Barua pepe: ……
4. Nchi ambako venia inapelekwa:
……
5. Sehemu (kituo cha forodha) shehena ya venia inapopita:
……
6. Kiwango kwa Mita za Ujazo: .....

Jina la Mwombaji:
……
Wadhifa: ……..
Saini:
……..

Tarehe: ……..
Muhuri wa Kampuni: ……

FOMU NAMBA 3

KIBALI CHA USAFIRISHAJI WA VENIA KWENDA NJE YA NCHI

Kibali kimetolewa kwa .....wa sanduku la posta …….....cha kusafirisha venia kwenda nchi ya .....kupitia bandari/uwanja wa ndege/kituo cha…….

(i) Spishi ya venia: ……..……
(ii) Mita za Ujazo: ……
(iii) Tarehe ya kutolewa kibali: ……

Jina: ……
Saini: …….
Kamishna wa Uhifadhi
Tarehe: .....

FOMU NAMBA 4

CHETI CHA UKAGUZI WA VENIA KWENDA NJE YA NCHI

Mimi……Nathibitisha kuwa nimekagua shehena ya venia inayomilikiwa na ……. iliyopo…….na kubaini kuwa imekidhi masharti yaliyotolewa chini ya Sheria za Misitu, Sura ya 323.
Leo tarehe ……Mwezi…….20…….

…….
Saini ya Afisa Mkaguzi

FOMU NAMBA 5

CHETI CHA KUSAFIRISHA VENIA NJE YA NCHI

Cheti hiki kimetolewa kwa..... wa sanduku la posta ..... kusafirisha Venia kutoka bandari/uwanja wa ndege/kituo cha ……kwenda nchi ya……kama ifuatavyo:

(a) Spishi ya venia: .....
(b). Mita za Ujazo: .....

Jina: ……
Saini: ……
Kamishna wa Uhifadhi

Tarehe: ……

Dodoma,
5 Septemba, 2024

PINDI HAZARA CHANA
Waziri wa Maliasili na Utalii